

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA HAMSINI NA SABA**

**28 JUNI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA HAMSINI NA SABA – TAREHE 28 JUNI, 2023**

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**748. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO  
(MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, nini hatma ya madai ya maslahi ya waliokuwa Wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**749. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA  
ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kabla Zahanati haijafunguliwa inawekewa Vifaa Tiba.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**750. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kuhusu hewa ya ukaa ili Wananchi waelewe na wanufaike na elimu hiyo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**751. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itafanya Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ili kuweka Tozo tofauti kulingana na ukubwa wa chombo cha moto.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**752. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa changamoto za biashara za Mpakani hasa utitiri wa Tozo.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**753. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna maamuzi mengine baada ya Kamati ya Mawaziri 8 kurudisha kwa Wananchi wa Itigi Shamba la Kampuni ya Tanganyika Parkers.

**WIZARA YA AFYA:**

**754. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza vifo vya Watoto wenye umri kati ya Sifuri hadi Mwaka Mmoja.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**755. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaruhusiwa kukusanya na kuitumia *Passenger Service Charge* kuboresha Viwanja vya Ndege.

**756. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Bunju B – Mabwepande – Kibamba utaanza.

**WIZARA YA MAJI:**

**757. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Wananchi wangapi wa Wilaya ya Kyerwa wamefikiwa na huduma ya maji safi na salama.

**WIZARA YA KILIMO:**

**758. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani kupitia SIDO kutoa mashine ndogo na rahisi kwa Vikundi vya Wanawake vya ubanguaji Korosho - Mtwara.

**759. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kilimo cha Minazi nchini.

**760. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itawachukulia hatua Viongozi wa Vyama vya Msingi waliodhulumu fedha za Wakulima wa Kahawa - Mbozi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**761. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Wanafunzi wangapi waliopata ujauzito wamerejea Shuleni tangu Waraka wa kuwaruhusu utolewe.

### **III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2023.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2023*].

### **IV. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**

### **V. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU:**

### **VI. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI.**

**DODOMA  
28 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**